

Behewa kwa jina lingine ni **UA**, ni eneo la wazi lililokuwa limezungushiwa fensi mbele ya Hema ya kukutania , kwa ajili ya makuhani kutoa sadaka za kuteketezwa, na kufanya shughuli za kikuhanzi tazama picha juu..

Lakini baadaye Hekalu lilipokuja kutengenezwa na Sulemani pale Yerusalem, eneo la behewa/Ua lilizungushiwa ukuta, na pakawa na behewa kuu mbili, 1) ya ndani 2) na ya nje, ili ya ndani ikabakia kuwa ya makuhani tu, kufanya mambo ya upatanisho na sadaka za kuteketezwa, Na ile ya nje ikabakia kuwa ya Wayahudi wote kukutanika kuabudu..Tazama picha chini..



Lakini pia behewa, kwenye biblia haikumaanisha tu ni lazima iwe mbele ya hema ya kukutania au mbele ya Hekalu la Mungu, biblia inayonyesha pia, zilikuwa pia kwenye majumba ya kifalme na ya kikuhanzi.

1 Wafalme 7:1 "Naye Sulemani alikuwa katika kujenga nyumba yake mwenyewe miaka kumi na mitatu, akaimaliza nyumba yake yote....11 Na juu kulikuwa na mawe ya thamani, mawe ya kuchongwa, sawasawa na cheo, na mierezi.

12 Na behewa kubwa pande zote ilikuwa na safu tatu za mawe ya kuchongwa, na safu moja ya mihimili ya mierezi; mfano wa behewa ya ndani ya nyumba ya Bwana, na ukumbi wa nyumba".

Mathayo 16:3 "Wakati ule wakuu wa makuhani, na wazee wa watu, wakakusanyika katika behewa ya Kuhani Mkuu, jina lake Kayafa";

Lakini pia katika kitabu cha ufunuo tunasoma, kuwa wakati wa mwisho, behewa/ua iliyo nje ya hekalu ambalo litakuja kujengwa na Wayahudi pale Yerusalem siku za mwisho, litamilikiwa na watu wa mataifa kwa muda wa miezi 42..

Ufunuo 11:1 “Nikapewa mwanzi kama fimbo; na mmoja akaniambia, Inuka, ukalipime hekalu la Mungu, na madhabahu, na hao wasujuduo humo.

2 Na behewa iliyo nje ya hekalu uiache nje wala usiipime, kwa maana Mataifa wamepewa hiyo, nao wataukanyaga mji mtakatifu miezi arobaini na miwili”.

Ili kufahamu habari kamili, sababu na maana yake rohoni ya mambo hayo fungua vichwa vingine vyta masomo tulivyovirodhesha chini.

Kwa mawasiliano/mafundisho zaidi kwa njia ya whatsapp, tutumie ujumbe kwenye namba hizi: +255789001312/ +255693036618

**Au Jiunge na magroup yetu ya whatsapp kwa kubofya hapa >
Group-whatsapp**

Mada Nyinginez

Konzo la Ng'ombe ni nini? (Waamuzi 3:31).

Hema ya kukutania ni nini, na ilikuwaje?

UBATIZO NI NINI NA ULIOSAHIHI NI UPI?

NA TAA YA MUNGU ILIKUWA BADO HAIJAZIMIKA

Je! dhambi zote ni sawa Kuna dhambi kubwa na ndogo?

Kisiwa cha Patmo kipo nchi gani?.

Rudi Nyumbani:

Share on:

WhatsApp